Lengo la Mwongozo huu ni kuwasaidia wale wote watakaohusika katika mafunzo ya uandaaji wa mipango ya shule. Mwongozo huu pia utatumika wakati wa mchakato wenyewe wa kuandaa mpango wa shule. Uandaaji wa mpango wa shule unaweza kufanyika kwa kushirikiana na wazazi, watumishi wa serikali, na wanachama wa vyama vya kijamii, viongozi wa jamii, walimu wote pamoja na wanafunzi. Serikali ya Tanzania inakasimu majukumu yake mengi kwa mamlaka za serikali za mitaa ikimaanisha kwamba wale walio katika ngazi ya shule itawabidi kuwajibika zaidi katika uendeshaji wa shule yao. Mafunzo yanahitajika kwa wawezeshaji na washiriki katika uandaaji wa mipango ya uboreshaji wa elimu ili waweze kupata maarifa, stadi na ulewa wa kufanikisha lengo hili.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) ambao umekuwa ukitekelezwa kwa ufanisi hapa Tanzania tangu mwaka 2002, ni mpango wa miaka mitano na una vipengele vikuu vinne:-

- a). Kuongeza uandikishaji wa wanafunzi
- b). Kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunzia.
- c). Kujenga uwezo katika mfumo wa elimu na katika sekta zingine za serikali na za wadau binafsi katika utoaji wa elimu.
- d). Kuimarisha miundo ya kiutawala na kiutendaji inayosaidia katika uandaaji mipango na utoaji wa huduma za elimu.

Uandaaji mipango ya elimu ni moja ya shughuli kuu katika kipengele cha "kujenga uwezo" na umuhimu wa kuandaa mpango kwa kutumia njia ya ushirikishwaji umesisitizwa sana katika MEM. Walimu wakuu wanahimiza kushirikiana na kamati za shule katika utoaji na urekebishaji wa mara kwa mara wa mipango ya miaka mitatu ya maendeleo ya shule pamoja na mipango yake ya utekelezaji ya mwaka. Ruzuku ya matumizi na ile ya maendeleo zitatolewa kwa shule ambazo zimeandaa mipango hiyo ipasavyo.

Yaliyomo

SEHEMU YA 1

WARSHA YA UANDAAJI MPANGO WA SHULE	1
NINI KINAENDELEA KATIKA ELIMU?	2

SEHEMU YA 2

MCHAKATO WA UANDAAJI MPANGO WA SHULE	5
HATUA MUHIMU KATIKA UANDAAJI MPANGO WA SHULE.....	5
HATUA 1: UCHAMBUZI WA WADAU	8
HATUA 2: UCHAMBUZI WA MATOKEO YA URAMANISHAJI SHULE	10
HATUA 3: UCHAMBUZI WA UUFV	16
HATUA 4: UUNDAJI PROGRAMU	18
4-1 KUWEKADIRA	18
4-2 KUWEKA MALENGO	19
4-2-1 Orodha ya Malengo ya Awali	19
4-2-2 Kubainisha Mapato	21
4-2-3 Kuweka Vipambebe vya Malengo	26
4-3 KUWEKA SHABAHA.....	28
4-4 UPANGAJI SHUGHULI	29
4-5 KUBAINISHA MAHITAJI	31
HATUA 5: MPANGO WA UTEKELEZAJI.....	34
HATUA 6: MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MWAKA.....	36
HATUA 7: MPANGO WA UFUATILIAJI.....	38

SEHEMU YA 3

KURIPOTI	40
KIAMBATISHO: NAMNA YA KUKOKOTOA VIASHIRIA VYA ELIMU	

SEHEMU YA 1

UTANGULIZI WARSHA YA UANDAAJI MPANGO WA SHULE

Uandaaji wa mpango wa shule siyo tu jitihada ya shule katika kujiboresha lakini pia ni jitihada ya jamii nzima katika kuboresha mazingira ambayo shule hiyo imo. Kutokana na mchakato wa mpango wa shule jamii inapata fursa yakuelewa hali halisi ndani ya shule na nje ya shule.

Washiriki katika kuandaa mpango wa shule ni pamoja na wale wote wanaojali maendeleo ya elimu ya msingi wakiwemo walimu wakuu na walimu wote, wazazi, wanafunzi, viongozi wa vijiji, viongozi wa kata na wengineo. Hivyo basi warsha inatakiwa kuitishwa ili wahusika wote wakutane na kuandaa mpango kwa pamoja.

Mwalimu mkuu atakuwa mwezeshaji wa warsha ya kuandaa mpango wa shule kwa kuratibu na kuongoza mjadala ambapo mwenyekiti wa kamati ya shule atakuwa mwenyekiti wa warsha hiyo. Kila mshiriki ana haki sawa ya kutoa mawazo yake, na kwa kawaida washiriki hufanya mjadala na kutoa michango yao katika vikundi ili kutumia vizuri muda mchache walio nao.

Mchakato wa kuandaa mpango wa shule unahitaji ushirikiano wa dhati kutoka kwa washiriki wote. Washiriki wana jukumu kubwa katika uandaaji wa mpango wa shule na wakati huo huo mwalimu mkuu anatakiwa asiegeme upande wowote na wala asilazimishe mawazo yake ila aratibu na kuongoza mjadala ili washiriki waandae mpango kwa utulivu.

Ikiwa mjadala wa mada fulani utarefushwa sana na mwalimu mkuu akaona kuwa mjadala si sahihi na unaenda mbali au nje ya mada hapo anaweza kuingilia kati na kuwaelekeza washiriki kwenye hatua inayofuata.

NINI KINAENDELEA KATIKA ELIMU?

MMEM NA F&VM (O & OD)

Kabla ya kuanza kuandaa mpango wa shule, washiriki wanatakiwa kujua jinsi mpango wa shule unavyohusiana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na utaratibu wa mipango kwa kutumia Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (F & VM) au kwa kiingereza "Opportunities and Obstacles to Development" (O & OD).

1 -1 Uandaaji mipango katika MMEM

Uandaaji wa mpango wa shule ni moja ya mikakati muhimu katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ambao ni mpango wa taifa wa miaka mitano kwa ajili ya elimu ya msingi. Kwa mujibu wa MMEM (2002 - 2006) uandaaji wa mpango wa shule unachukuliwa kama moja ya mikakati katika kujenga uwezo na kuboresha shule. Maelezo yaliyoko kwenye kisanduku hapo chini yametafsiriwa kutoka kwenye Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM).

1. Watumishi na wadau wote wenye majukumu ya moja kwa moja ya uendeshaji wa MMEM watapewa mafunzo ili kuhakikisha kuwa wanapata ujuzi wa upangaji mipango shirikishi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini, na uchangiaji katika uchanganuzi na utungaji wa sera.
2. Walimu wakuu watashirikiana na Kamati za Shule katika kuiandaa na kuifanyia marekebisho ya mara kwa mara mipango ya miaka mitatu ya maendeleo ya shule. Mipango hii ndiyo itakuwa msingi wa maamuzi yote yanayohusu maendeleo katika ubora na utoaji wa elimu, na ujenzi wa majengo mapya shuleni.
3. Kamati za shule zitapewa mafunzo kuhusu majukumu yao mapya.

1-2. Majukumu ya Kamati za shule kama yalivyobainishwa katika MMEM.

Kuna majukumu makuu tisa ya Kamati za shule yalivyobainishwa katika MMEM, nayo ni:-

1. Kuhisisha na kuwahusisha wanafunzi wote, wazazi na watumishi wote wa shule katika majukumu wanayoweza kutekeleza kwa masilahi ya shule ya msingi.
2. Kusimamia masuala ya siku hadi siku ya shule.
3. Kushirikiana na Mwalimu Mkuu pamoja na walimu wengine katika kuandaa mpango wa maendeleo ya shule.
4. Kuidhinisha Mipango ya Maendeleo ya Shule na Bajeti na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Maendeleo ya Mtaa, au Halmashauri ya Kijiji na halafu kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata na mwishowe kwenye mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya kuipitia, na kuiunganisha, na hatimaye kuiwasilisha kwenye Sekretariati za Mikoa.
5. Kuwezesha uandaaji wa mipango, bajeti na utekelezaji wa shughuli zinazogharimiwa na MMEM.
6. Kufungua akaunti benki na kusimamia vizuri na kwa ufanisi matumizi ya fedha zinazopokelewa kwa ajili ya utekelezaji huku ikijihakikishia uwajibikaji na uwazi wa hali ya juu katika mchakato uliotumika ikiwemo uwekaji bayana wa mapato na matumizi.
7. Kuhakikisha usalama wa mali na vifaa vilivyonunuliwa kwa fedha za MMEM.
8. Kuandaa na kuwasilisha kwa wakati ripoti sahihi za maendeleo na fedha kwa halmashauri ya kijiji, kamati ya maendeleo ya mtaa, na mamlaka za serikali za mitaa.
9. Kuwasilisha kwa ufasaha taarifa za elimu kwa wazazi wote, wanafunzi, wadau katika jamii, na kwenye kijiji, kata/mtaa na mamlaka za serikali za mitaa.

1 -3. Fursa na Vikwazo Kwa Maendeleo (F&VM).

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambayo inatekeleza MEM kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Utamaduni (WEU) inaanzisha mfumo shirikishi wa upangaji mipango unaojulikana kama Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (F & VM) au "Opportunities and Obstacles to Development" (O & OD) kwa kiingereza. Upangaji wake huanzia katika ngazi ya jamii (i.e. kijiji) kwa kutumia mipango shirikishi jamii au kwa kiingereza Participatory Rural Appraisal (PRA). Mpango huu ni mpana na unahusisha vipengele vingi katika jamii. Elimu ni moja tu ya vipengele hivyo.

Kimsingi Mpango wa Maendeleo wa Kijiji/Mtaa unatakiwa kutumika kama rejea wakati shule katika kijiji/mtaa huo zinaandaa Mipango ya Maendeleo ya Shule. Kwa mtazamo huu, Mpango wa Maendeleo wa Shule unakamilisha Mpango wa Maendeleo wa Kijiji/Mtaa pamoja na mchakato wa F & VM (O & OD).

SEHEMU YA 2

MCHAKATO WA UANDAaji MPANGO WA SHULE HATUA MUHIMU KATIKA UANDAaji MPANGO WA SHULE

Uandaaji mpango wa shule una ngazi mbili:-

Ngazi ya Uchambuzi wa hali halisi na ngazi ya kuandaa mpango. Ngazi ya uchambuzi wa hali halisi inahusu uchambuzi wa wadau, uchambuzi wa matokeo ya uramanishaji shule, na uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vikwazo vya shule. Ngazi ya kuandaa mpango inahusu Kuunda Programu, Mpango wa Utekelezaji, kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka na Mpango wa Ufuatiliaji.

Hatua ya kwanza ni Uchambuzi wa Wadau. Katika hatua hii washiriki watabainisha wadau wa shule na majukumu yao na umuhimu wao katika kuendeleza shule.

Hatua ya pili ni Uchambuzi wa Uramanishaji Shule (School Mapping analysis). Washiriki watachambua matokeo ya zoezi la uramanishaji shule na kubainisha hali halisi ya shule kwa kuangalia pia tofauti ya viashirio mbalimbali vya kielimu kati ya shule na malengo ya taifa.

Hatua ya tatu ni Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vikwazo (UUFV). Hapa washiriki watachambua hali ilivyo kwa kuzingatia uwezo, udhaifu, fursa na vikwazo kwa maendeleo ya shule.

Hatua ya nne ni Kuunda Programu. Katika hatua hii mwelekeo wa majadiliano unahama kutoka uchambuzi wa hali halisi ya shule na kuelekea kwenye namna ya kuboresha hali ya sasa ili kufikia "hali ya shule inayotarajiwa kwa wakati ujao". Hatua hii ina vipengele vya uwekaji wa Dira (visheni), uwekaji wa malengo, uwekaji wa vipaumbele vya malengo, uwekaji wa shabaha, ubainishaji wa shughuli na mahitaji yake, na ukokotoaji wa gharama kwa kila shughuli.

Hatua ya tano na ya sita zinahusu uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji na Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka. Mpango wa Utekelezaji ni matriki ya mpango wa miaka mitatu ambao huonyesha wazi "Malengo", "Shabaha", "Shughuli", "Chombo cha utekelezaji", "Mahitaji", "Gharama" na "Ratiba ya Utekelezaji". Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka ni mpango unaoonyesha

May 6, 2004 - Draft


shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa kwanza wa mpango. Kila mwaka mpango mwingine wa utekelezaji utaandaliwa kwa kuzingatia maendeleo ya mpango wa mwaka uliotangulia.

Hatu ya saba ni utayarishaji wa Mpango wa Ufuatiliaji, ambao huonyesha namna ya kufuatilia utekelezaji wa mpango wa shule.

Mwisho, baada ya warsha, Mwalimu Mkuu akishirikiana na Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, ataandaa rasimu ya mpango wa maendeleo ya shule. Baada ya kupitiwa kwa uangalifu na Kamati ya Shule, rasimu hiyo ya mpango itawasilishwa kwa mkutano wa Kijiji/Mtaa kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

May 6, 2004 - Draft

HATUA MUHIMU ZA KUANDAA MPANGO WA SHULE





UCHAMBUZI WA WADAU

Lengo: Kubainisha wale wanaotakiwa kushiriki katika kutatua matatizo ili kuboresha shule yetu.

Wadau ni nani?

Maamuzi mengi yaliyokuwa yanafanywa katika ngazi ya taifa kwa sasa yanafanywa katika ngazi ya jamii/kijiji. Shule, jamii na vijiji vinahimizwa kuchukua majukumu zaidi katika kupanga, kuendesha, kugharamia na kutekeleza parogramu na mifumo ya kielimu. Hii inahitaji ushiriki hai kwa kila mmoja ikiwepo kujunga na asasi mbalimbali katika ngazi ya shule na kijiji ambazo zimeanzishwa kwa lengo hilo. "Kila mmoja" inamaanisha wadau. Wadau ni wale wote wenye maslahi fulani katika matokeo ya elimu.

Shughuli na:

Kuorodhesha Majina ya Wadau wa Shule yetu.

Wadau wa shule yetu ni nani? Hebu tujadili na kuorodhesha wadau wa shule yetu.

•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•
•	•



Ni nini matarajio ya wadau?

Baada ya kubainisha wadau, sasa ni wakati wa kufikiria nini matarajio yao kuhusu shule. Kwa kutumia fomu ifuatayo tujadili na kuorodhesha matarajio mengi inavyoweza kwa kila mda.

Wadau	Matarajio
1.	
2.	
3.	
4.	
5.	
6.	
7.	
8.	
9.	

HATUA YA 2

UCHAMBUZI WA MATOKEO YA URAMANISHAJI SHULE

Lengo: Kujua hali ya shule ilivyo kwa sasa kwa kupitia uchambuzi wa hojaji za zoezi la Uramanishaji shule

Kutokana na ushiriki wenu katika masuala ya shule mnajua hali halisi ya shule, lakini inawezekana msijue iko katika hali nzuri au mbaya kiasi gani.

Matokeo ya zoezi la uramanishaji shule yatakuwezesheni kupata data kamili kuhusu hali ya shule. Mnaweza pia kugundua masuala mahsusi ya shule mkichunguza kwa makini matokeo ya hojaji za uramanishaji shule Sehemu ya 1 - 3. Vifuatavyo ni vichwa vya habari vya hojaji za uramanishaji shule ambazo matokeo yake tunayo:-



Hojaji za Uramanishaji shule

- Hojaji sehemu ya 1: Kuhusu Shule
- Hojaji sehemu ya 2: Kuhusu Walimu
- Hojaji sehemu ya 3: Kuhusu Wanafunzi

Shughuli na 3

Pengo ni kubwa kiasi gani kati ya malengo ya kitaifa na hali halisi ilivyo katika shule kwa sasa?

Hojaji sehemu ya kwanza inatoa data za shule. Tutumie data hizo kwa kujaza KARATASI YA UBAINISHAJI PENGO na kuangalia jinsi tarakimu zinavyokaribiana au kuwa mbali na zile zilizo katika malengo ya kitaifa. Ukiona tofauti kubwa kati ya takwimu za shule na zile za kitaifa weka alama ✓ katika safu ya mwisho. "Namna ya kukokotoa Viashirio" iko katika KIAMBATISHO kwa rejea yako.

KARATASI YA UBAINISHAJI PENGO

Viashirio	Shule yako	Malengo ya Kitaifa	Ukubwa wa Pengo
1. Kiwango halisi cha uandikishaji (NER)		100% (Hotuba ya makadirio)*	
2. Kiwango ghafi cha uandikishaji (GER)		100%	
3. Kiwango cha watoto walio nje ya shule.		0% (Hotuba ya makadirio)*	
4. Kiwango cha mahudhurio.		100% (walimu na wanafunzi)	
5. Uwiano kati ya wanafunzi na walimu.		40:1 (Hotuba ya makadirio)*	
6. Kiwango cha kuacha shule (Mondoko)		3% (Hotuba ya makadirio)*	
7. Kiwango cha kufaulu mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi		50% (Hotuba ya makadirio)*	
8. Kiwango cha kujiunga sekondari ya umma		50% (Hotuba ya makadirio)*	
9. Uwiano kati ya wanafunzi na vitabu		1:1	
10. Uwiano kati ya wanafunzi na darasa		40:1 (Hotuba ya makadirio)*	
11. Uwiano kati ya wanafunzi na matundu ya chao		25:1 (Wavulana) 20:1 (Wasichana)	
12. Uwiano kati ya wanafunzi na madawati		1:2 (Hotuba ya makadirio)*	
13. Uwiano kati ya Walimu na nyumba		1:1	
14. Sifa za Walimu		Daraja A zaidi ya 50%	
15. Maji safi		Ndiyo yawepo	
16. Uwanja wa michezo.		1 kwa shule	
17. Maktaba		1 kwa shule	
18. Meza (darasani)		1 kwa darasa	
19. Viti (darasani)		1 kwa darasa	
20. Makabati		1 kwa darasa	
21. Silabasi		1 kwa somo	
22. Kiongozi cha Mwalimu		1 kwa somo	
23. Ukubwa wa shule		Kijijini wanafunzi 560 Mjini wanafunzi 840	** ***

* Hotuba ya Waziri wa Elimu Mh. J.J. Mungai (MB) kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka 2003/2004

** Si zaidi ya mikondo miwili kwa darasa (40 x 2 x 7 = 560).
*** Si zaidi ya mikondo mitatu kwa darasa (40 x 3 x 7 = 840).



Hali ya Shule ikoje kwa sasa?

Sasa ebu, tuangalie matokeo ya hojaji sehemu ya 2 - 3 na pia data kutoka Hojaji sehemu ya 1 ambayo haimo katika Karatasi ya Ubainishaji Pengo. Jedwali lifuatalo linaonyesha muhtasari wa hojaji hizo. Pitia kila sehemu ya hojaji, bainisha hali ya shule ilivyo kwa sasa na uielezee katika Jedwali la hali ilivyo sasa shuleni lililoonyeshwa baada ya jedwali hili.

Muhtasari wa Hojaji Sehemu 1 - 3

Shule (Hojaji sehemu ya 1*)	Kuhusu mikondo na shifti mbili (S 6)
	Kuhusu magonjwa sugu na madawa ya kulevya (S 17 -19)
	Kuhusu usafiri na umbali kwenda shule (S 20 - 22)
	Kuhusu MEMKWA (S 26)
Maoni ya Walimu (Hojaji sehemu ya 2)	Kuhusu kupenda kwao kufundisha (S 1 - S 4)
	Kuhusu ufundishaji mzuri (S 5 - S 9)
	Kuhusu masuala ya UKIMWI (S 10 - S 12)
Maoni ya Wanafunzi (Hojaji sehemu ya 2)	Kuhusu kupenda kwao shule na masomo (S 1 - S 6)
	Kuhusu kujifunza vizuri (S 7 - S 8)
	Kuhusu kuacha shule na adhabu (S 9 - S 11)
	Kuhusu UKIMWI (S 12)
	Kuhusu upatikanaji wa chakula (S 13 - S 15)

* Taarifa ambazo hazimo katika Karatasi ya Ubainishaji Pengo.

HALI ILIVYO KWA SASA Muhtasari kuhusu Shule (Hojaji sehemu ya 1*)

Kuhusu mikondo na shifti mbili (S 6)

Kuhusu magonjwa sugu na madawa ya kulevya (S 17 -19)

Kuhusu usafiri wa mwanafunzi kwenda shule (S 20 - 22)

Kuhusu MEMKWA

* Taarifa ambazo hazimo katika Karatasi ya Ubainishaji Pengo.

Muhtasari wa mawazo ya Walimu (Hojaji sehemu ya 2)

Kuhusu kupenda kwao kufundisha (S 1 - S 4)

Kuhusu ufundishaji mzuri (S 5 - S 9)

Kuhusu masuala ya UKIMWI (S 10 - S 12)

Muhtasari wa maoni ya wanafunzi (Hojaji sehemu ya 3)

Kuhusu kupenda kwao shule na masomo (S 1 - S 6)

Kuhusu kujifunza vizuri (S 7 - S 8)

Kuhusu kuacha shule na adhabu (S 9 - S 11)

Kuhusu UKIMWI (S 12)

Kuhusu kupata chakula (S 13 - S 15)

IKHATUUA YA 3

UGHAMBUZI WA UWEZO, UDHAIFU, FURSA NA VIKWAZO (UUFV)
Lengo: Kujua hali halisi ya shule kwa sasa kwa kubainisha Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vikwazo.

Baada ya kuwatambua wadau na hali halisi ya shule kama ilivyo sasa hebu tu jaribu kubainisha Uwezo na Udhaifu wa shule na kuchunguza sababu za nje zinazoleta Fursa na Vikwazo. Uchambuzi huu unajulikana kama UUFV au SWOT (Strengths, Weakness, Opportunities and Threats) kwa lugha ya kiingereza na utawasaidia kuzingatia masuala muhimu katika kuandaa mpango wa shule.

Shughuli na.5

Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vikwazo vya shule ni vipi?

Tafadhali kila mshiriki aorodheshe kwanza Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vikwazo vingi inavyowezekana vya shule yake. Kisha msememe na kujadili yale mliyoorodhesha kama kikundi. Jedwali lifuatalo linaonyesha mfano wa jinsi ya kujenga uchambuzi wa UUFV (SWOT).

Mfano: Mfumo wa UUFV katika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Shule	
Uwezo	<ul style="list-style-type: none"> + Shule yetu ina madarasa ya kutosha + Jamii yetu inapendelea maendeleo ya shule yetu. + Shule yetu ina meza na viti vya kutosha. + Shule yetu ina uongozi mzuri.
Udhaifu	<ul style="list-style-type: none"> + Shule yetu haina walimu wa kutosha + Jamii yetu haina vitabu vya kutosha . + Shule yetu ina upungufu wa madawati na viti. + Shule yetu haina uwanja wa michezo kwa wanafunzi.
Fursa	<ul style="list-style-type: none"> + Kijiji chetu kina maeneo wazi karibu na shule + Kijiji chetu kina misitu mingi kwa ajili ya kutengeneza samani za shule.
Vikwazo	<ul style="list-style-type: none"> + Wanakijiji hawapendelei kuwapeleka watoto wa kike shuleni + Wanafunzi na familia katika kijiji chetu wana uelewa mdogo kuhusu UKIMWI. + Wazazi wengi wanaamini kuwa adhabu ya viboko ni muhimu kwa maendeleo ya elimu.

Uchambuzi wa UUFV wa shule yako.

Uwezo	
Udhaifu	
Fursa	
Vikwazo	

UUNDAJI PROGRAMU

Lengo: Kuunda mpango kwa kuweka Dira, malengo, shabaha kwa kila lengo na kubainisha shughuli na mahitaji kwa kila shughuli.

Hadi sasa mmefanya uchambuzi wa wadau, uchambuzi wa uramanishaji shule na uchambuzi wa UUFV. Sasa mtaingia katika hatua nyingine, Uundaji wa Programu.

Hatua hii inahusu uwekaji wa dira, uwekaji wa malengo na vipaumbele vyake, uwekaji wa shabaha, ubainishaji wa shughuli na rasilimali inayohitajika na ukokotoaji wa gharama kwa kila shughuli.

4.1. KUWEKA DIRA

Kabla ya kuingia katika kiini cha Uundaji Programu ambacho ni Uchambuzi wa Malengo, mtahitajika kuweka Dira au Lengo kuu la shule.

Dira ni nini? Dira ni "picha ya wakati ujao". Tamko la Dira lazima liwe wazi na linalowezekana na lazima lionyeshe mwelekeo wa mpango. Kwa nini "Dira" inahitajika? Kwa sababu haiwezekani kuchagua malengo na vipaumbele vyake bila kuwa na dira (Visheni). Dira itaonyesha mwelekeo wa shule.

Shughuli na 6.

Dira ya shule yenu ni nini?

Tafadhali jadilini katika vikundi vidogo kuhusu dira ya shule yenu inavyoweza kuwa. Hii ni hatua muhimu kwani dira ndiyo shabaha ya malengo na shughuli zote mtakazopanga. Sasa mtashirikisha mawazo yenu na kisha kuamua dira inayofaa kwa shule yenu.

DIRA YA SHULE YETU**4-2. KUWEKA MALENGO**

Malengo wazi na yanayotekelezeka huwekwa kwa kutumia mchakato wa "Uchambuzi wa Malengo". Uchambuzi wa malengo ni mchakato wa kubaini hali nzuri itakayofikiwa mara baada ya utatuzi wa matatizo ya sasa na kuweka sawa mbinu na mahusiano yanayotakiwa ili kufikia hali hiyo.

4-2-1. Orodha ya Malengo ya Awali.

Kabla ya kubainisha malengo ya mwisho washiriki wataweka malengo ya awali. Orodha ya malengo ya awali inaweza kupatikana kutokana na uchambuzi wa hali halisi. Uchambuzi wa hali iliyopo umeonyesha pengo lililopo kati ya ngazi ya shule na ngazi ya kitaifa. Kwa kuzingatia uchambuzi, washiriki watatengeneza orodha ya malengo ya awali ambayo yatafanikisha dira (visheni).



Ni Malengo yapi ya kufanikisha Dira?

Ebu, tujaribu kuandaa orodha ya malengo. Jedwali lifuatalo linawapeni baadhi ya mawazo. Wakati mnaamua na kuweka malengo katika orodha ya awali ni vizuri mzingatie uwezekano wa utekelezaji wa kila lengo kwa kuangalia mbinu za utekelezaji. Zaidi ya hapo lazima mhakikishe kuwa mbinu zitakazotumika zinatekelezeka na kwamba kila lengo halitaleta madhara yoyote wakati wa utekelezaji.

Mfano: Orodha ya malengo ya awali:

**DIRA: SHULE YETU ITAWAPATIA WATOTO WOTE KIJIJINI
FURSA SAWA YA ELIMU BORA YA MSINGI.**

Malengo ya awali	Mbinu
1. Wanafunzi wengi watakuwa na vitabu	Kuomba wilaya kusambaza vitabu zaidi shuleni.
2. Vifaa vya kutumia shuleni vitaongezeka.	Kukarabati madarasa yaliyopo. Kujenga madarasa mapya. Kutengeneza samani zilizoharibika
3. Wazazi watawapeleka shule watoto wao ambao hawajapata kwenda shule	Kuwa na mikutano na wanakijiji, wazazi na walimu kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi.
4.	
5.	
6.	

ORODHA YA MALENGO YA AWALI

Malengo ya awali	Mbinu
1.	
2.	
3.	
4.	
5.	
6.	
7.	
8.	
9.	
10.	
11.	
12.	


4-2-2. Kubainisha vyanzo vya mapato:

Kabla ya kuweka malengo ya mwisho hatuna budi kubainisha vyanzo mapato yanayohitajika kwa utekelezaji wa shughuli zitakazotakiwa ili kufikia malengo. Kuna vyanzo vikuu viwili vya mapato kwa ajili ya maendeleo ya shule yetu, ambavyo ni Serikali na Jamii.

A. Fedha za Serikali:


Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002 - 2006 unasema kwamba serikali inazipatia shule aina mbili za ruzuku. Ruzuku ya Matumizi (Capitation Grant) na Ruzuku ya Maendeleo (Development Grant). Ruzuku ya matumizi hutumika kwa ajili ya kununulia vitabu na vifaa vingine vinavyoongeza ari ya kujifunza na kufundisha na vifaa vingine ambavyo siyo mishahara lakini huchangia kuboresha mazingira ya kusoma na kujiifunza.

<Yaliyomo katika Ruzuku ya Matumizi>



Ruzuku ya Maendeleo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa na vifaa vya usafi.

<Yaliyomo kwenye Ruzuku ya Maendeleo>



Ruzuku ya Matumizi:

Mwanafunzi mmoja kama Tshs. 10,000
Fedha ya matumizi ya shule yako ni = Tshs 10,000 x namba ya wanafunzi katika shule

(Mfano)

Ununuzi wa vitabu:	TSh. 4,000 @ mwanafunzi
Ukarabati wa vifaa na Samani:	TSh. 1,980 @ mwanafunzi
Kununua vifaa vya kufundishia:	TSh. 1,980 @ mwanafunzi
Gharama za uendeshaji:	TSh. 1,020 @ mwanafunzi
Kuendesha mitihani:	TSh. 1,020 @ mwanafunzi
Jumla	TSh.10,000/-

Fedha za Maendeleo:

Kabla ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MEM)



Ujenzi wa madarasa



Uligharimiwa na wazazi

Baada ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MEM)



Ujenzi wa madarasa



Unagharimiwa na wazazi

Ujenzi wa Madarasa



Ruzuku ya Maendeleo
Kutoka serikalini (2TShs. 4,000,000)

Mchango wa jamii
+ Fedha (Taslimu)
+ Nguvu kazi
+ Vifaa

Sharti la kupewa
ruzuku ya Maendeleo

B. Mchango wa Jamii:

Kama inavyoeleweka, ada ya elimu ya msingi imefutwa. Serikali inazikataza shule kuomba fedha kwa wazazi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Serikali kuu, kupitia serikali ya Wilaya, inatoa Rukuzu ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Hata hivyo kuna sharti moja ambalo ni lazima litekelezwe kabla ya kupokea Ruzuku ya Maendeleo toka Serikalini - *Mchango wa jamii*. Mchango huu unaweza kuwa ni fedha taslimu, nguvukazi au vifaa vya ujenzi.



Kuandaa Mawazo ya kuhamasisha jamii.

Maelezo yaliyotolewa hapo juu yanaonesha kuwa uhamasishaji wa jamii ni muhimu na njia bora za mawasiliano zinatakiwa ili kubaini njia za kuongeza vyanzo na viwango vya mapato ya shule. Katika uhamasishaji jamii, kamati za shule zitatakiwa kuchukua majukumu na kudhihirisha uwezo wao wa ubunifu na ujasiriamali.

Mawazo mazuri kuhusu mchango wa jumuiya

Hili ni zoezi la kubunga bongo ambapo kikundi kizima kitatoa mchango wa mawazo ambayo mwezeshaji atayaandika ubaoni. Hakuna majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mara baada ya kukamilisha orodha (walao mawazo 10) lazima kila wazo lijadiliwe. Ni vizuri kufikiri kwanza kabla ya kuamua kwa haraka kuwa jambo fulani haliwezekani. Baada ya kumaliza mjadala, andikeni mawazo mnyoona yanafaa kufanyiwa majaribio katika shule yenu.

Mfano:

Mawazo mazuri sana	Mambo ya kuzingatia ili mawazo mazuri yanikiwe
1. Kuendesha kampeni za kutambua umuhimu wa elimu.	Wajumbe wa kamati ya shule, wazazi, wanafunzi na wanajamii kwa ujumla wafanya matembezi ya hisani kijijini.
2. Kuiendea halmashauri ya Kijiji.	Wajumbe wa kamati ya shule wajiunge katika mkutano wa halmashauri ya kijiji, watoe maelezo kuhusu utaratibu wa fedha za maendeleo zilizotolewa na MEM na kuwomba wajumbe wa halmashauri ya kijiji kuunga mkono mpango wa maendeleo wa shule
3. Kuchangisha fedha	Wajumbe wa kamati ya shule, wazazi pamoja na wanafunzi watembelee nyumba za matajiri kama vile wafanyabiashara na kuomba mchango.
4. Kuchangisha fedha	Kukiwa na matamasha au sherehe za kidini/mikutano ni nafasi nzuri za kukusanya mchango.

May 6, 2004 - Draft

Mawazo mazuri sana	Mambo ya kuzingatia
1.	
2.	
3.	
4.	
5.	
7.	
8.	
9.	
10.	

C. Vyanzo vingine

Shule yenu inaweza kuwa na vyanzo vingine vya mapato. Baadhi ya shule zina miradi yao kama vile bustani ya mboga, miradi ya korosho, ambayo huipatia shule kiasi fulani cha mapato. Mapato hayo yatiliwe maanani wakati wa kuandaa mpango wa shule.



Kutayarisha Karatasi ya Ubainishaji Mapato

Ni muhimu kwenu kujua vyanzo vya uhakika vya mapato ambavyo shule inaweza kukusanya wakati wa kuandaa mpango. Hebu tuorodheshe aina za mapato ya miaka iliyopita kutoka vyanzo mbalimbali. Andikeni aina zote za mapato. Ni vizuri kama mtatafsiri michango yote ya nguvukazi au hali katika thamani ya fedha, lakini kama ni vigumu mnaweza kuandika aina na kiasi cha mchango (nguvukazi kwa ujenzi ya watu 20 kwa siku 28, kilo 50 za mchanga n.k.)

May 6, 2004 - Draft

Mwaka 2002

Aina ya Mapato	Chanzo	Kiasi	Matumizi
Ruzuku ya Matumizi	Serikali		
Ruzuku ya Maendeleo	Serikali		
Mchango wa jamii	Jamii		
Jumla			

Mwaka 2003

Aina ya Mapato	Chanzo	Kiasi	Matumizi
Ruzuku ya Matumizi	Serikali		
Ruzuku ya Maendeleo	Serikali		
Mchango wa jamii	Jamii		
Jumla			

Mwaka 2004

Aina ya Mapato	Chanzo	Kiasi	Matumizi
Ruzuku ya Matumizi	Serikali		
Ruzuku ya Maendeleo	Serikali		
Ruzuku wa jamii	Jamii		
Jumla			

Kutokana na mahesabu hapo juu sasa mtaweza kukisia kiasi cha mapato ya shule ambayo shule inaweza kukusanya kwa kipindi cha mpango 2005 - 2007. Yaandikeni katika Karatasi ya Ubainishaji Mapato.

Karatasi ya Ubainishaji Mapato (2005-2007)

Aina ya Mapato	Chanzo	Kiasi			
		2005	2006	2007	Jumla
Ruzuku ya Matumizi	Serikali				
Ruzuku ya Maendeleo	Serikali				
Mchango wa jamii	Jamii				
Jumla					

4-2-3. Kuweka Vipambebe vya Malengo

Kwa kutumia orodha ya malengo ya awali ambayo mlitengeneza na ubainishaji wa mapato mliofanya katika hatua iliyopita, sasa ni muda wa kuyapa vipambebe malengo ya awali. Malengo yaliyopewa vipambebe yapewe maelezo wazi na vielelezo vinavyoonyesha hali ilivyoboreka baada ya utekelezaji. Malengo yaliyowekewa vipambebe yatatakiwa kupangwa na kupewa namba kwa kuzingatia vipambebe.



Kuyaweke malengo vipambebe:

Ebu, tuanze kwa kupitia orodha ya malengo ya awali tuliyoorodhesha katika shughuli iliyopita. Kama kikundi mtaamua ni lengo lipi muhimu zaidi kuliko mengine, yaani kipaambebe cha kwanza. Andika namba 1 mbele yake. Halafu amueni ni lipi lenye umuhimu wa pili na andika namba 2 mbele yake. Endeleeni kufanya hivyo hadi malengo yote yamalizike. Mnaweza kuamua kubadilisha mpangilio wakati wowote. Itabidi mtengeneze utaratibu wa namna ya kukubaliana kwa kuwa itabidi kufikia muafaka kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho.

Baada ya kumaliza kuyaweke malengo vipambebe chunguzeni tena orodha. Mnadhani mnaweza kuchukua malengo yote katika Mpango wa Maendeleo ya shule wa miaka mitatu au kuacha mengine kutokana na muda mfupi na mapato haba? Tafadhali jadilini tena orodha kwa kuzingatia ukweli huu na kukamilisha jedwali lifuatalo kwa kuandika upya malengo kwa mpangilio wa vipambebe. Orodhesheni malengo yale tu ambayo mmeamua kuyaweke katika mpango wa miaka mitatu.

Malengo kwa Vipambebe

1.
2.
3.
4.
5.
6.
7.
8.
9.

4-3 KUWEKA SHABAHA

Mmechagua malengo ya mpango na kuyapatia vipaumbele sasa mtaweka shabaha wazi kwa kila lengo kwa kutumia Viashirio Bainifu.

"Bainifu" ina maana kwamba mtu yeyote anaweza kucheki tena na kupata matokeo yale yale. Viashirio vya aina hiyo vitawawezesheni kupima kwa usahihi mafaniko au maendeleo ya malengo. Viashirio bainifu vitatumika pia kama vigezo vya ufuatiliaji na tathmini hapo baadae.

Hapa chini ni muundo na mfano wa Karatasi la Viashirio. Viashirio vinatakiwa kuchaguliwa kwa makini ili viweze kupima mafanikio au maendeleo ya lengo na viwe rahisi kupatikana. Mnaweza kupata viashirio zaidi ya kimoja kwa kila lengo.

Mfano: Karatasi ya Viashirio

Malengo	Viashirio Bainifu				
	Aina ya Data	Hali ya sasa	Shabaha kila mwaka		
			2005 mwishoni	2006 mwishoni	2007 mwishoni
<Lengo 1> Watoto wote kijijini watahudhuria shule.	Kiwango halisi cha uandikishaji (NER)	85%	90%	95%	100%
	Kiwango cha watoto nje ya shule	15%	10%	5%	0%
<Lengo 2> Vifaa matumizi shuleni vitaongezeka	Uwiano wa wanafunzi /darasa	76/1	60/1	50/1	45/1
	Idadi ya madarasa yanayotumika	6	8	9	10
	Uwiano wa wanafunzi/madawati	5/1	4/1	3/1	3/1
	Idadi ya madawati yanayotumika	90	120	150	160
	Uwiano wa Wanafunzi/vyoo	Wav. 50/1 Was. 56/1	32/1 32/1	30/1 26/1	25/1 20/1
	Idadi ya vyoo vinavyotumika	Wav. 5 Was. 4	7 7	8 9	10 12
<Lengo 3> Shule itatoa elimu bora zaidi.	Kiwango cha kufaulu MKEM	12%	15%	20%	25%
	Uwiano walimu/wanafunzi	64/1	60/1	50/1	45/1
	Idadi ya walimu	7	8	9	10
	Kiwango cha kwenda sekondari	4%	8%	10%	20%
<Mengine yameachwa >					



Utayarishaji wa Karatasi la Viashirio


Kwa kutumia muundo hapo juu tayarisheni Karatasi la Viashirio. Kwanza mtaandika malengo yote katika safu ya kushoto. Halafu mtajadili na kupata viashirio vinavyofaa kwa kupima mafanikio ya malengo. Mnatakiwa kwanza kutaja hali halisi iliyobainishwa kutokana na zoezi la uramanishaji shule, na kisha mtaweka shabaha zinazotekelezeka. Karatasi la ubainishaji Pengo mliloliandaa awali (uk. 11) linaweza kutumika kama rejea mnapoweka shabaha. Kulingana na hali halisi ya shule yenu pamoja na upungufu wa muda na mapato ya shule yenu, kwa wakati huu mnaweza kulazimika kuweka shabaha ambayo ni chini ya shabaha ya taifa. Shabaha zinatakiwa ziwe zile zinazotekelezeka. Kwa kuwa mpango ni wa miaka 3 mnatakiwa kuweka shabaha zinazoweza kufikiwa kila mwaka.

4- 4. UPANGAJI SHUGHULI

Shughuli ni vitendo mahsusi vinavyohitajika kutimiza malengo kwa kutumia vizuri rasimili zilizopo. Kwa mfano ili kutimiza lengo "Vifaa vya matumizi shuleni vitaongezeka" vitendo mbalimbali vinatakiwa kufanyika kama vile ukarabati wa vyumba vya madarasa, ukarabati wa samani iliyoharibika, ununuzi wa samani mpya, n.k. Vitendo hivi ndiyo "shughuli". Kwa vile inatubidi tubainishe mahitaji na gharama ya kila shughuli katika hatua inayofuata, shughuli zinatakiwa kuandikwa kwa ukamilifu na uwazi inavyowezekana. Kwa mfano, "jenga vyumba vipya vya madarasa," "nunua vitabu vya kiada" au "andaa mkutano" haiwapi taarifa ya kutosha kuweza kubainisha mahitaji ya rasimili. Kwa upande mwingine, "Jenga madarasa 4 mapya," "Nunua vitabu vya kutosha vya Hisabati kwa madarasa 5 - 7 ili watoto 3 wachangie kitabu kimoja" au "andaa mikutano kila mwezi" itawapatieni kigezo cha kubainisha mahitaji na kukokotoa gharama.

Shughuli zinatakiwa kuorodheshwa kufuatana na muda wa utekelezaji kama zinatekelezwa kwa mfuatano huo. La siyoy ziorodheshwe kwa mpangilio wa vipaumbele.

Fomula ya kukokotoa gharama (bajeti)



Kama rejea, vifuatavyo ni viwango vya bei zilizoandikwa katika "Micro Planning 2002-2006" Wizara ya Elimu na Utamaduni (WEU) na UNICEF mwezi Septemba 2001.

Kipengele	Bei yake (Sh)
Ujenzi mpya	
Darasa	4,000,000
Nyumba ya mwalimu	5,000,000
Ofisi ya Walimu	2,000,000
Maktaba	4,000,000
Vyoo	173,100
Stoo	2,000,000
Chumba cha wanafunzi wa kike	4,000,000
Matengenezo	
Darasa	1,009,000
Nyumba ya mwalimu	1,202,000
Samani	
Dawati la wanafunzi	6,000
Kiti cha mwanafunzi	4,000
Rafu	60,000
Meza	4,600
Kitalu cha maua	70,000
Vifaa vya kufundishia	
Kitabu cha Hesabu	1,200
Kitabu cha Kiswahili	2,600
Kitabu cha kujisomea	1,000
Mafunzo kazini	300,000

Ufuatao ni mfano wa Orodha ya Mahitaji na ukokotoaji wa gharama za shughuli kwa kutumia bei zilizoonyeshwa hapo juu.

INA	Shughuli	Mahitaji	Ukokotoaji wa Gharama
2.1	Karabati madarasa 2 yaliyopo	Vifaa, nguvukazi, seremala	Tshs. 1,009,000 x 2 = Tshs. 2,018,000
2.2	Jenga madarasa 4 mapya	Fundi mwashi, vifaa, nguvukazi.	Tshs. 4,000,000 x 4 = 16,000,000
2.3	Jenga vyoo 5 vya wavulana na 8 vya wasichana	Fundi mwashi, vifaa nguvukazi	Tshs. 173,100 x 13 = 2,250,300
2.4	Nunua madawati 70	Mwalimu Mkuu, fedha za kununulia madawati	Tshs. 6,000 x 70 = Tshs. 420,000.



Ukokotoaji wa makadirio ya Gharama

Sasa kazi yenu ni kupata bei za kila kipengele kinachotakiwa kwa shughuli mlizobainisha katika hatua iliyotangulia.

Orodha ya Bei za kila kipengele

Vipengele	Bei (Tshs.)

Kwa kutumia bei mlizopata hapo juu sasa mnaweza kukokotoa gharama ya kila shughuli mkitumia muundo hapo chini. Kwanza mtaandika shughuli zote zilizobainishwa katika Jedwali la Malengo na Shughuli (uk. 30) halafu muandike mahitaji yote (watu na vifaa) na kukokotoa gharama ya kila shughuli.

Orodha ya Mahitaji

	Shughuli	Mahitaji	Ukokotoaji wa Gharama
1.1			
1.2			
1.3			
<inaendelea>			

MFANO: MPANGO WA UTEKELEZAJI

Tina la Shule xxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

Muda: Jan 1, 2005 - Des. 31, 2007

Tmeandaliwa 15 Aug. 2004

Dira: Shule yetu itawapatia watoto wote kijijini fursa sawa ya elimu bora ya msingi.

Malengo	Shabaha	Shughuli	Chombo cha Utekelezaji	Mahitaji	Gharama	Ratiba ya Utekelezaji		
						2005	2006	2007
Lengo 1 Watoto wote wa umri wa kawanda shule kijijini watahuhuria shule	Kiwango halisi cha Uondikishaji (NER) 100%. Kiwango cha watoto nje ya shule 0%	1.1	Itisha mikurano 3 ya Uhamasishaji katika kijiji	Kamati ya Shule				
		1.2	Patia kila mtoto dhakula cha mchana	Kamati ya Shule	Kiongozi wa kijiji	Tsh. 22mil.		
Lengo 2 Vifaa vya matunzizi viraongezeka	Uwiano wa warafunzi/darasa wa 45:1	2.1	Nunua mipira kwa kila darasa na andaa muda wa michezo kila wiki	Kamati ya Shule	Wazazi, Unga Mboga	Tsh. 90,000		
		2.2	Karabati madarasa 2 yaliyopo.	Kamati ya Shule	Wazazi, walimu Mipira 15	Tsh. 2,018,000		
	Uwiano wa warafunzi/dawati wa 3:1	2.3	Jenga madarasa 4 mopya	Fundi mwishi, vifaa, nguvukozi	Tsh. 16,000,000			
		2.4	Jenga vyo 5 vya wawilana na 8 vya wasichana	Kamati ya Shule	Fundi mwishi, vifaa, nguvukozi	Tsh. 2,250,000		
			Nunua madawati 70	Kamati ya Shule	Mwalimu Mkuu, Fedha za kumundia madawati 70	Tsh. 420,000		



MPANGO WA UTEKELEZAJI
Lengo - Kuandaa mpango wa utekelezaji ambao ni muhtasari wa namna na lini shughuli husika zitekelezwe katika miaka mitatu ilayo.

Kutokana na hatua za Uundaji Programu mmeweza kuchagua na kuyapatia vipaumbele malengo, kuweka shabaha, kubainisha shughuli na mahitaji. Sasa tutaunda Mpango wa Utekelezaji (MU), ambao unatoa muhtasari wa namna na wakati wa kutekeleza mpango. Vipengele vyake muhimu ni pamoja na malengo, shabaha, shughuli, chombo cha utekelezaji, mahitaji, gharama na ratiba ya utekelezaji.

Safu ya kwanza na ya tatu zina malengo na shughuli ambavyo mmekwisha orodhesha katika Jedwali la Malengo na Shughuli (ukurasa wa 30). Safu ya pili ni shabaha ambazo mmeziandika katika Karatasi la Viashirio. Safu ya nne ni kwa ajili ya Chombo cha Utekelezaji. Mtabainisha nani atawajibika kwa utekelezaji wa kila shughuli. Safu ya tano, Mahitaji, ni kwa ajili ya mahitaji ya watendaji na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa kila shughuli na katika safu ya mwisho mtabainisha muda wa utekelezaji. Mfano wa mpango wa utekelezaji umeonyeshwa katika ukurasa unaofuata.

Shughuliya ya 14 Kuandaa Mpango wa Utekelezaji

Sasa mtaandaa Mpango wa Utekelezaji kwa kutumia muundo ulioonyeshwa katika ukurasa unaofuata.

MFANO: MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MWAKA

Jina la Shule: xx

Muda Januari 1, 2005 - Desemba, 31, 2005

Umeandaliwa: Agosti 15, 2004

	Shughuli	Chombo cha utekelezaji	Mahitaji	Gharama	Chanzo	Ratiba ya Utekelezaji (2005)			
						R1	R2	R3	R4
1.1	Ilisho mlikotano kuhamasisha madhuhuro shuleni	Kamati ya shule	AMK (VEO) Maandilizi ya mlikotano ya kijiji						
1.2	Andaa kikundi cha kutoa chakula cha mchana mpira kile mchana shuleni	Kamati ya shule	Wazazi Unga Mboga (katoka bustani ya shule) Wazazi	Tsh. 7,000,000	Shule				
1.3	Nunua mipira kwa oroda muda wa michezo kila wiki	Shule	Majimu Mpira IO	Tsh 60,000	Jamii				
2.1	Karabati madarasa 2 ya vyopo	Kamati ya shule	Vifaa Nguvukazi Seremba	Tsh 1,000,000 Tsh 700,000 Tsh 318,000	Serikali Kuu Jamii Serikali Kuu				
2.2	Jenga madarasa 2 mpya	Kamati ya shule	Fundi mwaazi Vifaa vya majali Nguvu kazi	Tsh 2,000,000 Tsh 2,000,000 Tsh 800,000	Wiliyoa Serikali Kuu Jamii				
2.3	Jenga vyoo 2 vya wastahona vya wastahona	Kamati ya shule	Fundi mwaazi Vifaa vya majali Nguvu kazi	Tsh 100,000 Tsh 405,500 Tsh 150,000 Tsh 210,000	Wiliyoa Serikali Kuu Jamii				
2.4	Nunua madawati 30	Shule Jamii	Mawilimu Mkuu Fedha za kumunika madawati	Tsh 180,000	Serikali Kuu				

MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MWAKA
Lengo: Kutayarisha mpango wa utekelezaji wa mwaka ambao ni muhtasari wa namina na lini utekelezaji wa shughuli husika utafanyika

Kutokana na mpango wa utekelezaji wa miaka mitatu ijayo uliotayarishwa katika hatua iliyotangulia, mpango wa utekelezaji wa mwaka utaandaliwa. Mpango wa utekelezaji wa mwaka ni mpango wa undani zaidi kwa mwaka mmoja wa kwanza wa mpango (kwa upande wetu ni 2005). Shughuli zile tu ambazo zimepangwa kwa ajili ya mwaka husika ndizo zinatakiwa kuonyeshwa kwa uwazi katika mpango wa utekelezaji wa mwaka husika. Kwa mfano, mpango wenu ni "Kujenga madarasa 4 mapya" katika miaka 3 ya mpango (ukurasa 35, shughuli 2.2 ya Mpango wa Utekelezaji). Ikiwa mtajenga madarasa 2 katika mwaka wa kwanza, mpango wa utekelezaji wa mwaka (kwa mwaka wa kwanza) utataja "jenga madarasa 2 mapya" (ukurasa 37 shughuli 2.2 ya Mpango wa mwaka wa Utekelezaji). Mnaweza kuona mfano ukurasa unaofuata.



Uandaaji wa Mpango wa Mwaka wa Utekelezaji

Sasa mtaandaa Mpango wa Mwaka wa Utekelezaji mkifuata muundo ulioonyeshwa katika ukurasa unaofuata.

Hili si zoezi gumu kwani mpaka sasa mna taarifa za kutosha. Tumieni mfano wa mpango wa utekelezaji wa mwaka ulioko katika ukurasa unaofuata kwa shughuli hii.

HATUA YA 7

MPANGO WA UFUATILIAJI

Lengo: Kutayarisha mpango wa ufuatiliaji ikiwa ni muhtasari wa namna gani ilini na nini kifuatiliwe

Ufuatiliaji ni kubaini kiwango cha utekelezaji wa programu na kurekebisha mpango kama ni lazima. Kiwango cha mafanikio ya shughuli na malengo huangaliwa upya wakati wa ufuatiliaji. Ili kutekeleza jukumu hili barabara inatakiwa kuwa na Mpango wa Ufuatiliaji. Mfano wa mpango wa ufuatiliaji umeonyeshwa katika ukurasa unaofuata.

Shughuli na. 16

Kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji

Mpango wa Ufuatiliaji unatakiwa kuonyesha *Malengo* ambayo utekelezaji wake unatakiwa kufuatiliwa na *Aina ya Data* itakayotumika katika kupima mafanikio na pia *Shabaha* za kila lengo na viashirio vyake bainifu. Hivyo vimekwisha bainishwa katika ukurasa uliotangulia. Mnachotakiwa ni kunakili kwanza malengo na viashirio kutoka katika Karatasi ya Viashirio.

Zaidi ya hayo mtu atakayewajibika na ukusanyaji wa taarifa, mbinu na mara ngapi kuripoti, na mtu wa kuhakiki ripoti anatakiwa kubainishwa.

MFANO: MPANGO WA UFUATILIAJI

Jina la Shule: xxxxxxxxxxxxxxxx Muda: Januari 1, 2005 - Desemba 31, 2007
Imetayarishwa Agosti 25, 2004

Malengo	Aina ya Data	Viashirio Bainifu				Mkusanyaji Taarifa	Mbinu na mara za kuripoti	Mhakiki Ripoti
		Hali Halisi sasa	Shabaha ya kila mwaka					
			Mwisho wa 2005	Mwisho wa 2006	Mwisho wa 2007			
Lengo 1 Watoto wote kijijini wa umri wa kwenda shule watahudhuria shule	Kiwango cha Uandikishaji (NER)	85%	90%	95%	100%	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	Kiwango cha watoto nje ya shule	15%	10%	5%	0%	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
Lengo 2 Vifaa vya matumizi shuleni vitaongezeka	Uwiano wa wanafunzi/ darasa	76:1	60:1	50:1	45:1	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	Idadi ya modarasa yanayotumika	6	8	9	10	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	Uwiano wa wanafunzi/ dawati	5:1	4:1	3:1	3:1	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	Idadi ya madawati yanayotumika	90	120	150	160	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	Uwiano wa wanafunzi/vyoo	Wav. 50:1 Was: 56:1	32:1 32:1	30:1 26:1	25:1 20:1	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	Idadi ya vyoo vinavyotumika	Wav. 5 Was. 4	7 7	8 9	10 12	Mwalimu mkuu	Ripoti ya Shule Kila robo mwaka	Kamati ya Shule, MEK
	<mengine yameachwa>							

SEHEMU YA 3

KURIPOTI

Baada ya kumaliza hatua na ngazi zote katika warsha, Mwalimu mkuu akishirikiana na Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, ataunganisha pamoja matokeo yote ya warsha katika Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Shule. Baada ya kukamilika rasimu ya mpango huo inatakiwa kupitiwa kwa uangalifu na Kamati ya Shule na kuwasilishwa kwenye Kijiji/Mtaa na baadaye kwenye Kata na Wilaya.

Muundo wa Mpango wa Maendeleo wa Shule umeonyeshwa katika ukurasa unaofuata.

MUUNDO WA MPANGO WA MAENDELEO WA SHULE

Majumuisho Rasmi

(Eleza kwa kifupi mchakato wa kuandaa mpango na toa muhtasari wa uchambuzi wa Hali Halisi, Dira, Malengo na gharama yote ya kutekeleza Mpango wa miaka 3 wa maendeleo wa Shule).

1. Hali ya Shule kwa sasa

1.1: Matokeo ya Uchambuzi wa wadau

(Toa Muhtasari wa Wadau wa Shule na matarajio yao).

1.2: Matokeo ya uramanishaji Shule

(Toa Muhtasari wa matokeo ya uramanishaji shule na ambatanisha Karatasi la Ubainishaji Pengo).

1.3: Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vikwazo vya Shule

(Toa muhtasari wa uwezo, udhaifu, fursa na vikwazo vya shule).

2. Uundaji wa Programu

2.1: Dira

(Andika Dira na eleza jinsi dira iliyopatikana).

2.2: Malengo

(Ambatanisha Orodha ya vipaumbele vya malengo na jinsi malengo yalivyopatikana na kupewa vipaumbele).

2.3: Shabaha

(Ambatanisha Karatasi la Viashirio)

2.4: Shughuli na Mahitaji

(Ambatanisha Karatasi la Ubainishaji wa Mapato, orodha ya bei na orodha ya mahitaji).

3. **Mpango wa Utekelezaji**
(Ambatanisha Mpango wa Utekelezaji. Hakuna haja ya maelezo).
4. **Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka**
(Ambatanisha Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka bila maelezo zaidi).
5. **Mpango wa Ufuatiliaji**
(Ambatanisha Mpango wa Ufuatiliaji bila maelezo zaidi).
6. **Viambatanisho:**
Taarifa zozote muhimu kwa kusaidia yaliyomo kwenye ripoti.

Kiambatisho

NAMNA YA KUKOKOTOA VIASHIRIA VYA ELIMU

Kiwango halisi cha uandikishaji au Net Enrolment Rate (NER) kwa kiingereza.

Hiki huonyesha asilimia ya watoto wa umri wa kwenda shule walioko shuleni kati ya idadi ya watoto wote wa umri huo huo. Kwa mfano kama kijijini kwako kuna watoto 200 wa umri wa shule (miaka 7 - 13) na kati yao 120 wamo shuleni tunaweza kusema kuwa NER ni 60%. Hii inaweza kukokotolewa kwa urahisi kama ifuatavyo:-

$$\begin{aligned} \text{NER} &= \frac{\text{Watoto wa umri wa shule walioko shuleni}}{\text{Watoto wote wa umri wa shule}} \times 100 \\ &= \frac{120 \times 100}{200} = 60\% \end{aligned}$$

NER ikiwa kubwa ni vizuri zaidi. Kama watoto wote wa rika la shule wako shuleni NER ni 100%. Hapa tunajumlisha wavulana na wasichana kwa pamoja. Ni vizuri pia kupata NER ya wavulana na wasichana peke yao kwa ulinganisho.

Kiwango ghafla cha uandikishaji au Gross Enrolment Rate (GER).

Hiki kinafanana na NER. GER huonyesha asilimia ya watoto wa umri wowote walioko shuleni kati ya rika lengwa la umri wa shule (7-13). Kwa mfano ikiwa katika kijiji chako watoto wa umri wa shule ni 200 na walioko shuleni (umri wowote) ni 160 tunaweza kusema GER ni 80%. Hii inaweza kukokotolewa kama ifuatavyo.

$$\begin{aligned} \text{GER} &= \frac{\text{Wanafunzi wote (umri wowote)}}{\text{Wanafunzi wa umri wa shule}} \times 100 \\ &= \frac{160 \times 100}{200} = 80\% \end{aligned}$$

May 6, 2004 - Draft

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa GER ikiwa kubwa ni vizuri zaidi lakini kwa upande mwingine ni vigumu kidogo kuielewa kwa sababu hapa tunalinganisha wanafunzi wote wa umri mbalimbali na watoto wote wa rika la shule. NER ni kipimo kizuri zaidi kwa kuangalia mwenendo wa uandikishaji wa watoto wa rika la shule. Lakini ni rahisi zaidi kupata GER kwa sababu hatuna haja ya kujua umri wa kila mwanafunzi. Tunaweza pia kujua mwenendo wa uandikishaji wa watoto kwa umri mkubwa/mdogo kwa kuangalia GER na NER kwa pamoja. Kwa mfano iwapo NER ni 60% na GER ni 80% inamaanisha nini? Katika kadhia hii tunaweza kusema kuwa kati ya wanafunzi wote, asilimia 20 ni ama chini ya umri wa miaka 7 au zaidi ya miaka 13.

Watoto nje ya shule (out of school children)

Hapa tuanafikiria juu ya aina mbili za watoto ambao hawako shuleni. Moja ni wale ambao wamefikia umri wa kuwa shuleni lakini hawako shuleni, na aina ya pili ni wale ambao wamevuka umri wa shule na hawakwenda shule au waliacha shule. Tunapofikiria juu ya aina ya kwanza ni rahisi kupata asilimia yao kwa sababu ni tofauti kati ya wanafunzi wote wa rika la shule na walioko shuleni wa rika hilo. Kwa mfano ikiwa NER ya kijiji chako ni 60% tunaelewa kuwa takribani 40% ya watoto wa rika la shule hawako shuleni. Ingawa hatuanguali wanafunzi wanaokwenda kusoma shule mjini au vijiji vingine tunaweza kuona ni asilimia ngapi ya watoto wa rika lengwa hawasomi shule kwa kuangalia NER. Bila shaka ikiwa ni wachache ni vizuri zaidi.

Ni vigumu zaidi kupata kiwango cha watoto wa umri mkubwa kuliko rika la shule kwa sababu ya tofauti iliyopo kati yao kiumri. Idadi yao inaweza kuhesabiwa kijijini. Hii ni muhimu kwa ajili ya mipango ya elimu isiyo rasmi na elimu ya watu wazima.

Kiwango cha mahudhurio au Attendance rate (AR)

Hiki ni tofauti na viwango vya uandikishaji. Hiki hutonyesha asilimia ya wanafunzi ambao huja shuleni na kuhudhuria masomo. Kwa mfano ikiwa wanafunzi 40 waliandikishwa darasa la 4 mwanzo wa mwaka na 10 hawahudhuri, hapa maana

May 6, 2004 - Draft

yake ni kwamba kiwango cha mahudhurio ni 75% ambacho hupatikana kama ifuatavyo:-

$$\text{Kiwango cha Mahudhurio} = \frac{\text{Wanafunzi wanaohudhuria}}{\text{Wanafunzi walioandikishwa}} \times 100 = \frac{40-10}{40} \times 100 = 75\%$$

Viwango vya mahudhurio vinaweza kukokotolewa kwa darasa au shule. Kwa kuwa mahudhurio hubadilika siku kwa siku ni kawaida kuchukua wastani wake. Kama unaovyojua kiwango kikiwa kikubwa ni vizuri zaidi.

Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu au Pupils Teacher Ratio (PTR)

Hii kwa kifupi huonyesha idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mmoja. Huu ni ulinganisho wa idadi ya walimu na ile ya wanafunzi.


Kwa mfano, ikiwa shule yako ina walimu 7 na wanafunzi 350, PTR ni 50, ambayo ni idadi ya wanafunzi gawanya kwa idadi ya walimu. Kufuatana na mwongozo wa WEU idadi ya wanafunzi 40 inapendekezwa kwa kila mwalimu.

$$\text{PTR} = \frac{\text{Wanafunzi wote}}{\text{Walimu}} = \frac{350}{7} = 50$$

Kiwango cha kuacha shule (Mdongoko) au Drop Out (DOR)

Hebu tuangalie darasa. Tufikirie tuna wanafunzi 25 katika darasa la 3. Kwa kawaida tunataka wote waingie darasa la 4 mwakani, lakini ukweli ni kwamba hilo haliwezekani kwa sababu baadhi ya wanafunzi wataacha kuhudhuria shule (drop out) na wengine watakariri darasa la 3 mwakani (repetition).

Drop Out Rate



Mwaka huu darasa la 3

Mwakani darasa la 4

Hebu tufikirie kadhia hapo juu. Watano (5) wanaacha kuja shule lakini 2 wanarejea na 3 wanaacha kabisa. Hapa kiwango cha kuacha shule (DOR) ni 12% ambacho kinapatikana ifuatavyo:-

$$DOR = \frac{\text{Wanafunzi (wanaoacha shule kabisa)}}{\text{Wanafunzi wote mwaka huu}} \times 100 = \frac{3}{25} \times 100 = 12\%$$


Bila shaka DOR ikiwa ndogo ni vizuri zaidi.

Ili kupata kiwango cha Mdongoko na ukariri tunahitaji kuangalia idadi ya wanafunzi kwa miaka miwili. Aidha kuna uwezekano kuwa wale 3 ambao hawakurejea shuleni huenda wamejiunga na shule nyingine. Kuwafuatilia si rahisi na kiwango cha

kuacha shule kinaweza kuathiriwa katika eneo dogo kama kijiji. Lakini matokeo ya kujiunga na shule nyingine hayana madhara katika kiwango cha taifa.

Kiwango cha kumaliza shule au Completion Rate (CR)

Kiwango hiki huonyesha asilimia ya wanafunzi wanaofika darasa la mwisho na kumaliza. Hebu tuangalie kielelezo hapa chini ili kuona maana ya kiwango cha kumaliza.



Kundi hili lilianza 1997 kama darasa la 1 likiwa na wanafunzi 50. Likawa darasa la 7 mwaka 2003 lakini idadi ya wanafunzi ilipungua kufikia 32 baada ya miaka 6.

$$CR = \frac{\text{Wanafunzi wanaomaliza katika kundi}}{\text{Wanafunzi waliokuwamo katika kundi}} \times \frac{32}{50} \times 100 = 64\%$$

Bila shaka asilimia ikiwa kubwa ni vizuri zaidi.

Kwa kawaida huenda baadhi ya wanafunzi walioanza 1997 wakakariri darasa na kumaliza miaka kadhaa baadaye. Hao si lazima wajumlishwe katika viwango vya kumaliza shule. Hata hivyo kufuatilia wale ambao wanakariri kunafanya ukokotoaji wa viwango kuwa mgumu.

Vile vile ni vigumu kidogo kufuatilia idadi ya wanafunzi katika kipindi cha miaka 6 iliyopita. Kiwango cha kumaliza kinaweza kupatikana kwa kuchukua idadi au viwango vya wanafunzi wanaopanda daraja katika madarasa 7. Ingawa hawa siyo sehemu ya kundi lengwa tunaweza kupata kiwango cha kumaliza ambacho kinaonyesha mwenendo wa upandaji daraja na umalizaji shule.

May 6, 2004 - Draft

MKEM (PSLE)

Huu ni mtihani ambao hufanywa na wanafunzi wa darasa la 7 kabla ya kumaliza shule. Wanafunzi hufanya masomo 4 na kupewa alama katika gredi 5 zinazoanzia na A na kumalizikia na E.

Wanafunzi wanaopata A,B,C huhesabiwa kuwa wamefaulu na wanastahili kuendelea na masomo ya sekondari. Mtihani huu huendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania ambayo ni taasisi chini ya WEU.

Hebu tunagalie shule ya kijijini pako. Ikiwa wanafunzi 5 walifaulu MKEM mwaka jana kati ya wanafunzi 25 wa darasa la 7 nini kiwango cha kufaulu MKEM?

Kiwango cha kufaulu MKEM = $\frac{\text{Wanafunzi waliofaulu}}{\text{Wanafunzi waliofanya mtihani}} \times 100 = \frac{5}{25} \times 100 = 20\%$
(PLSE Pass Rate) darasa la 7 mwaka jana.